***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kla nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Kunayo mambo ___**1**___ sana yanayofundishwa shuleni ___**2**___ elimu vitabu pekee. Kwanza, shuleni ___**3**___ humpa mwanafunzi nafasi ya kukutana na kutunga ___**4**___ wazuri na wabaya. Ni jukumu ___**5**___ kila mmoja kuchagua masahibu hao kwa ___**6**___. Wawe ni wale wasemwao kuwa, ___**7**___.

___**8**___ shuleni, wanafunzi hupata fursa ya kuvitambua vipawa vyao. ___**9**___, wote huzawidiwa nafasi bora zaidi ya kujifunza maadili na namna bora za kuishi na walimwengu wenzao.

1. A. mingi  B. nyingi  C. mengi  D. mwingi
2. A. licha ya  B. minghairi ya  C. mithili ya  D. mathalan
3. A. yenyewe  B. penyewe  C. hiyo  D. pia
4. A. mabui  B. mahasidi  C. majirani  D. wadarisi
5. A. ya  B. wa  C. la  D. za
6. A. mapuuza  B. machezo  C. masihara  D. makini
7. A. baada ya dhiki faraja  B. Akufaye kwa dhiki ndiye rafiku  C. leo ni leo msema kesho ni mwongo  D. Hasira harasa
8. A. Huko huko  B. Hukó huku  C. kuko huku  D. kuko huko
9. A. Isitoshe  B. Isipokuwa  C. Japo  D. Ilhali

___**10**___ siku zilivyosonga ___**11**___ tulivyozidi kujituma zaidi. Sote tulishikilia imani moja. Sharti ___**12**___ katika kurekebisha hali ambayo kwa sasa ilitishia kutupa kuenda nguu.

___**13**___ yetu ilisalia kuwa , "umoja ni nguvu." Ingawa ___**14**___ waliona ugumu, ___**15**___ na kuwahakikishia kuwa baada ya dhoruba huja ushwari.

10. A. kwa kuwa  B. Maadam  C. Kadri  D. Ndivyo
11. A. ndipo  B. ndiyo  C. ndio  D. ndivyo
12. A. tunyookewe  B. tulemewe  C. tuelemewe  D. tutofautiane
13. A. moto  B. kaulimbiu  C. usemi  D. maneno
14. A. Miongoni mwetu  B. Kati yetu  C. Ndani yetu  D. Baadhi yetu
15. A. tuliwatia shime  B. tuliwavunja moyo  C. tuliwakebehi  D. tuliwabwagia zani

*Kutoka swali la 16 - 30, jibu swali kulingana na maagizo.*

**16. Andika wingi wa ukubwa sentensi uliyopewa.**
Kidole chake kilivunjwa na mbuzi.
A. Madole yao yalivunjwa na mabuzi
B. Madole yake yalivunjwa na mabuzi
C. Vidole vyao vilivunjwa na mbuzi
D. Dole lake lilivunjwa na buzi.

**17.** Chagua orodha yenye vielezi pekee.
A. zuri, epesi, embamba, safi
B. kalamu, Nairobi, maji, chumvi
C. upesi, asteaste, kizamani, sana
D. haraka, zuri, polepole, mathalan

**18.** Mara nyingi unaweza kumkaribisha mwenye kosa vyema ajapo kwako. Makaribisho yako huenda yakamrekebisha. Ni methali gani ambayo inaweza kutumiwa kuelezea hali kama hii?
A. Jirani mui heri kuwa naye
B. Harubu harabu
C. Nzi hufia kidondani
D. Hasidi mpe kiti akae

**19.** Chombo cha ufundi cha mhunzi atumiacho kuwekelea chuma anachokifua huitwa
A. jiriwa
B. timazi
C. fuawe
D. tumbawe.

**20.** Nomino dhahania iliyoundwa kutokana na sifa ni
A. safi - usafi
B. vumilia - mvumilivu
C. cheka - ucheshi
D. sumbua - usumbufu.

**21.** Mawele, mabua, matete na malezi ni mifano ya nomino katika ngeli ya
A. LI - YA B. U ZI
C. U - YA D. YA - YA.

**22.** Tano ni kwa chokaa kama vile kicha ni kwa
A. mbwa B. kifunguo
C. nywele D. mboga.

**23. Andika katika usemi wa kuripoti.**
"Ukichezea elimu utajiharibia mustakabali wako. "Mshauri alisema.
A. Mshauri alisema kuwa ukichezea elimu utajiharibia mustakabali.
B. Mshauri alisema kuwa angeichezea elimu angejiharibia mustakabali wake.
C. Mustakabali wako utaharibika ikiwa utachezea elimu yako.
D. Mshauri alisema kuwa angechezea elimu mustakabali wako utaharibika.

**24.** Kizimba ni nyumba ya kuku vilevile kizimba ni
A. mahali anamowekwa mfungwa kutumikia kifungo chake
B. chumba kidogo katika kituo cha polisi
C. mahali asimamapo mshukiwa wakati wa kesi.
D. anamotiwa mshukiwa anapokana mashtaka.

**25.** Gani ni aina ya shairi?
A. Utenzi B. Ubeti
C. Ukwapi D. Diwani

**26. Kanusha:**
Kazi iliyowasilishwa imesahihishwa.
A. Kazi isiyowasilishwa imesahihishwa
B. Kazi haijawasilishwa haijasahihishwa
C. Kazi haikuwasilishwa na haijasahihishwa
D. Kazi iliyowasilishwa haijasahihishwa

**27. Tegua kitendawili kifuatacho:**
Ukimwona anakuona.
A. jicho B. miwani
C. kioo D. jua.

**28. Kamilisha sentensi.**
________ ningekuwa na uwezo ningekusaidia.
A. Ilhali B. Angalao
C. Lau D. Madhali

**29.** Sentensi gani iliyotumia kiambishi cha hali iliyopita muda si mrefu?
A. Mtaenda kucheza
B. Alipolala niliamka
C. Nimekuwa sokoni
D. Yeye huimba akiwa

**30.** Semi gani yenye maana ya **"kupoteza njia"?**
A. Chana mbuga
B. Kanyaga chechele
C. Ingiwa na chechele
D. Enda arijojo

***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Senga alikuwa mfano wa jisu shuleni pao. Ulimi wake ulimpa kusema kwa ufedhuli mwingi ajabu. Heshima na maneno ya adabu aliyasikia tu ila aliyakosea maana kabisa. "Bingwa" huyu wa matusi, lugha chafu, majibizano yasiyo na msingi wala mashiko aliogopewa nà kila mtu. Si watu pekee waliomwogopa, la hasha. Hata kuta na milango vyote vilimwogopa. Aliigonganisha milango yote kwa mshindo mkuu, si ya msalani si ya bwaloni si ya darasani! Alimradi alipiganisha na kuchonganisha wote na vyote kwa ustadi wa kipekee.

Wavyele wake Senga, Bwana na Bibi Toa walikuwa watu wenye nafasi na hali mtaani pao. Walikuwa wamejenga kasri moja lisilo na mfano katika janibu hizi zao. Kila jicho lililotua kwenye jumba hilo lilishuhudia ustadi mwingi wa ujenzi. "Lazima fundi-msanifu wa jengo hili ana akili nyingi" Waliishia kusema wapita njia. Japo kazi ya Bwana na Bi. Toa ilisalia siri yao wenyewe, zilikuwapo fununu na ufifi kwamba miaka ya nyumba wote waliwahi kuwa wanasiasa wakubwa katika nchi yao ya Kombozi. Huko ndiko mtu na bibiye walikokutana na kuamua kwanza familia pamoja.

Baada ya wawili hawa kuchukuana na kufanya akidi, walifululiza moja kwa fungate yao kule **ughaibuni.** Yakini, walitumia kima kikubwa mno cha mali kwa shughuli hiyo. Mungu ni wa wote. Aliwajaalia kitoto chao cha kiume. Wakakiita Senga. Na huyu Senga sasa ndiye alikuwa mwiba wenye ncha kali. Aliwanyima wote heshima. Mara nyingine ungemsikia hata akitolea wakubwa wake amri kalikali zilizowachoma kwa uchungu mkali lakini wafanye nini, maskini wa Mungu!

Siku zilikunjuka taratibu na kumpa Senga wetu nafasi ya kukua na kuwa nazi mbovu zaidi. Alishikwa sikio mara zote ila yeye alitemea mate kila aliloambiwa. Alikosa kabisa nafasi ya kupima ushauri wowote walau atathmini endapo lipo lolote la maana. Ya nini afanye hivyo? Mtu huishi leo, kesho ni ya Mungu. Na leo yake ilijaa uhai na maisha mazuri ya itisha- upewe. Mwisho wa yote, Senga alifikiwa na muda wake wa kufanya mtihani wa kitaifa kama wenzake wengine. Haikuwa ajabu kwake kushika mkia kwa alama zisizotajika kwa **aibu, soni na fedheha.**

Wazazi wake walitumia "ujuzi" wa mfuko kumtafutia nafasi ya kidato cha kwanza. Ingawa ilipatikana kwa taabu nyingi, haikusalia kwa muda mrefu. Senga alifukuzwa kabisa shuleni kutokana na tabia zake. Wakati huu ndipo familia hii ilitanabahi kwamba hakuna msiba usio na mwenziwe. Bwana na Bi. Toa wote walishtakiwa kwa kuyatumia mali ya umma ndivyo sivyo. Zaidi ya hayo, walipatikana na hatia ya kunyakua ardhi waliyojengea kwa njia za nyuma. Walitiwa nyuma ya nondo kwa miaka mitano na kazi ngumu. Senga alipigwa na maisha akapigika kwelikweli. Alibaki kurukwa na akili na kuvulia watu nguo katika soko la Sokomoko. Kila aliyemwona alimwambaa kama muwele wa maradhi makali ya kuambukiza.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza
A. Senga alikuwa mpyaro
B. Wazazi wa Senga waliwahi kuwa wanasiasa.
C. Walimu walipendezwa na Senga
D. Senga alitusi hata milango na kuta.

**32.** Kijana aliyesimuliwa angeelimishwa kwa kauli zote **isipokuwa**
A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
B. Zinguo la mtukutu ni fimbo
C. Mtaka unda hanadi
D. Heshima si utumwa

**33.** Hata kuta na milango vyote vilimwogopa! Hii ni tamathali gani ya lugha?
A. Sitiari
B. Chuku
C. Msemo
D. Takriri

**34.** Kwa mujibu wa kifungu **si kweli**
A. Bwana na Bi. Toa waliwajibikia malezi ya mwanao.
B. Maskini ya kina Senga ilikuwa ya kifahari
C. Wazazi wa Senga waliwahi kuwa wanasiasa
D. shughuli za kisiasa ziliwakutanisha baba na mama Senga.

**35.** Ughaibuni ni
A. ng'ambo
B. marekani
C. uropa
D. nchi za mbali.

**36.** Senga
A. wazazi na walimu wake walimchoka
B. alijirekebisha akawa mtoto mzuri
C. alifeli katika mtihani na maisha
D. hakujali wala kubali hadi alipohitimu na kufanikiwa maishani.

**37.** **Soni, fedheha** na **aibu** yote ni mifano ya
A. visawe
B. vitate
C. vitawe
D. vielezi.

**38.** Unafikiria kutumia **"ujuzi wa mfuko"** kunaweza kusimamiwa na kauli gani?
A. Kuchana mbuga
B. Kuzunguka mbuyu
C. Maji kuzidi unga
D. Kula kalenda

**39.** Wazazi wake Senga wanaweza kulaumiwa kwa sababu
A. walimpa mahitaji ya msingi
B. walikuwa mafisadi wazuri
C. walikosa kumpeleka Senga shuleni
D. walikosa kumrudi ili kumrekebisha Senga.

**40.** Kifungu kimethibisha kuwa
A. mwisho wa familia ya kina Senga haukuwa mzuri.
B. wazazi wa Senga waliishi vyema jelani
C. walimu waliumia sana alipofeli Senga
D. ardhi iliyonyakuliwa ilikuwa halali ya Bwana na Bi. Toa.

***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Je, umewahi kujiuliza ulimwengu wa kesho utakuwaje? Umewahi kuyafikiria **maisha ya kisogoni yalivyokuwa?** Ungehiari yapi?

Ukweli uliopo ni kwamba teknolojia imeyabadilisha maisha sana. Imeliweka daraja kubwa ajabu baina ya enzi za jana na za leo. Kwa mfano, binadamu siku hizi halazimiki kwenda safari za mbali ili kufanya manunuzi yake. Anaweza, badala yake, kubofya tu kwenye simu au tarakilishi au chombo chochote kile chenye uwezo wa kuingia mtandaoni na kuagiza vyote anavyohitaji. Baada ya muda fulani bidhaa zake zote zitawasilishwa.

Aidha uwepo wa mtandao umesaidia mno katika kuanika baadhi ya maovu ambayo yaliishi kufichika katika kiza cha maki. Kikubwa zaidi ni jinsi walimwengu wameunganishwa na kuwa kijiji kidogo tu. Masuala ya haki za kibinadamu yameshughulikiwa kwa njia ya kipekee. Elimu kuhusu masuala ibuka duniani vilevile imetolewa mtandaoni kwa kila mtu. Kufanya hivi kunawezesha kusambaa kwa maarifa muhimu miongoni mwa watu. Mathalan, magonjwa kama vile kansa, virusi vya Korona yamepata kupewa ufafanuzi wa kina mtandaoni. Hili limewafanya wengi kuelewa wafanye nini ili kupunguza makali na maambukizi zaidi.

Katika ujamii bora, mtandao umesaidia pakubwa kufanyiza michango muhimu. Kwa mfano katika kipindi cha wanafunzi wa kidato cha kwanza kujiunga na shule ya upili, wapo waliopata misaada ya kulipia karo hii. Alihitajika tu mtu mmoja kuliweka suala la aina hii mitandaoni hasa ya kijamii. Penye wabaya hapakosi wema. Wema hao hutuma michango yao kwenye nambari ya simu au akaunti iliyotolewa. Haba na haba bila shaka hujaza kibaba. Hatimaye karo au hitaji lililotajwa huwa limeshughulikiwa.

Usakaji haki mtandaoni pia haujaachwa nyuma. Yapo, kwa mfano, maovu kama vile mauaji, unyanyasaji na dhuluma anuwai ambazo zimepata hadhira kubwa mtandaoni. Hali kama hii hulazimisha shirika au idara lengwa kushughulika kwa uwajibikaji zaidi. Vilevile, hadhira hii hupalilia umoja ulimwenguni.

**Kizuri bila shaka hakikosi ila** . Ingawa kuna mengi ya kujivunia daraja hili lililotutoa katika ukale, yapo mengi yanayostahili kupigwa darubini. Mathalan, kumetokea "majambazi" watumiao mtandao kupora, kulaghai na kutapeli wengine. Zaidi ya hilo, pia hutoa vitisho kwa watumizi huku wakiwataka kulipa malipo ya ukombozi. Wengine hutumia mtandao kusambaza taarifa za chuki, uongo pamoja picha zisizokubalika. Wote hawa huuchafua mtandao na kuvuruga maadili. Yataka sheria kali kuwekwa ili kujikinga dhidi ya hawa. Aidha, ni vyema sisi wenyewe kujiimarisha kimaadili na kitabia ili sote tupate kuishi vyema katika dunia ya leo.

41. Aya ya kwanza imetumia fani gani ya lugha?
A. Methali
B. Balagha
C. Sitiara
D. Tasfida

42. **Maisha ya kisogoni** ni yapi?
A. Maisha ya sehemu iitwayo kisogo
B. Maisha ya kuishi nyuma siku zote
C. Maisha bila ya teknolojia yoyote
D. Maisha ya siku za nyumba zilizopita

43. Kwa mujibu wa kifungu
A. maisha ya nyuma yalikosa umoja
B. bora una mtandao maisha yako huwa raha
C. biashara imerahisishwa na mtandao
D. bidhaa za mtandaoni huwa ghushi

44. Gani si faida ya mtandao?
A. Umoja wa kilimwengu
B. Utapeli
C. Elimu ya masuala ibuka duniani
D. Ujamii bora

45. Aya ya nne inathibitisha ukweli kuwa
A. kuna uwezekano wa kuimarisha jamii
B. kuna watoto wanaokosa shule kwa karo
C. kuna watu wabaya wanaosaidia watoto kwenye mitandao.
D. kila hitaji linapotumwa kwenye mitandao ya kijamii ni sharti lishughulikiwe.

46. **Kizuri hakikosi ila**. Yaani
A. kitu kizuri huzidisha ubaya wake
B. wema na uovu huishi pamoja daima
C. ukiujua huum huujui huu
D. hakuna kilicho bora kikamilika lazimakiwe na walakini.

47. Si kweli kuwa
A. matapeli huwa mtandaoni pekee
B. mtandao ni hazina muhimu ya ulimwengu
C. matumizi mabaya ya mtandao hudhuru
D. elimu kuhusu masuala anuawai inaweza kutolewa kwa njia ya mtandao.

48. Njia **bora zaidi ya** kupiga vita uchafu mtandaoni ni
A. kuweka sheria madhubuti
B. kujiimarisha kimaadili na kitabia
C. kufunga jela watumizi wabaya wa mtu
D. kukatiza mawasiliano yote na wanaoshukiwa kuwa wachafuzi.

49. Dunia ya leo inahitaji
A. tulalie ujuzi wetu
B. tufumbie macho yanayofanyika duniani
C. kila mtu awe katika mtandao
D. twende na uchao.

50. Daraja ililotajwa hapa linamaanisha
A. televisheni
B. kompyuta
C. mtandao
D. werevu wa kutumia simu.